## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AJIRA MPYA ZA UALIMU NA KADA ZA AFYA

### 1. UTANGULIZI

**Ndugu Wanahabari**;

Mtakumbuka kuwa mwezi Aprili, 2022; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** alitoa kibali cha ajira kwa kada za Ualimu na Afya, kwa ajili ya kuajiri walimu **9,800** wa Shule za Msingi na Sekondari, na wataalam wa Afya **7,612**.

Baada ya kupata kibali cha ajira, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitoa tangazo kwa wahitimu mbalimbali wa Ualimu na Kada za Afya, kuwasilisha maombi ya kazi, kupitia mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kuchakata maombi ya ajira, kuanzia tarehe **20/04/2022 hadi 08/05/2022**. Jumla ya maombi **165,948** yakiwemo ya Wanawake **70,780** na Wanaume **95,168** yaliyopokelewa kwenye mfumo, ambapo maombi ya Kada za Afya ni **42,558,** na Kada ya Ualimu ni **123,390.**

**Ndugu Wanahabari;**

Ili kufanikisha mchakato wa ajira, Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliunda Timu Maalum, ya kufanya Uchambuzi wa Maombi ya Ajira, iliyohusisha Taasisi mbalimbali. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Baraza la Taifa la

Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET), Sekretarieti ya Ajira, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), na Mabaraza ya Kitaalamu katika Sekta ya Afya.

**(a) Vigezo Vilivyotumika**

**Ndugu Wanahabari**;

Kutokana na idadi ya waombaji kuwa kubwa, Timu ya Uchambuzi wa Maombi ya Ajira ilipewa vigezo vilivyoandaliwa kama mwongozo wa kutoa ajira kwa waombaji, kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa haki na uwazi katika zoezi hili. Katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa, katika vigezo vilivyotumika kupata waajiriwa wapya kwa mwaka 2022, kila kigezo kilizingatia uwiano wa kijinsia. Vigezo vilivyotumika ni kama ifuatavyo: -

**i. Mwaka wa kuhitimu**

Katika kigezo hiki, kipaumbele kimetolewa kwa waombaji wenye sifa waliotangulia kuhitimu kwa mfuatano wa mwaka, kulingana na hitaji la kada/kozi au kiwango cha Elimu, na pia mwaka wa kozi ilivyoanza kutoa wahitimu.

**ii. Umri wa kuzaliwa**

Waombaji wenye sifa waliopangwa kwa mujibu kigezo namba (i) hapo juu walipangwa kulingana na umri wa kuzaliwa. Lengo ni kuwawezesha waombaji wenye umri unaokaribia miaka 45 kuingia katika utumishi wa umma kwa masharti ya kudumu, kwa mujibu wa Sera ya Ajira Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma toleo la Pili la mwaka 2008.

### iii. Waombaji Wenye Ulemavu

Uchambuzi wa maombi ya watu wenye Ulemavu ulifuata vigezo vyote vya **mwaka wa kuhitimu** na **umri wa kuzaliwa,** vilivyooneshwa kwenye kipengele cha (i) na (ii). Hata hivyo, vigezo hivi vilitumika kuwashindanisha waombaji wenye ulemavu peke yao, kwa kuzingatia takwa la Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, kifungu cha 31 (1)-(3). Uchambuzi huu ulifanywa kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Ndugu Wanahabari**

Mchakato wa uchambuzi wa maombi ya ajira ya Kada za Afya na Ualimu ulizingatia utaratibu ufuatao:-

i. Kwanza, ilihusisha uchambuzi wa moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa maombi. Mfumo huu umewezesha waombaji wote wenye sifa kupata ajira kwa haki na usawa, kama yalivyo maelekezo ya Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita, **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** kwamba Watanzania wote wenye Sifa wapate ajira bila upendeleo. Hivyo mfumo huu uliwachuja waombaji awali kwa kuzingatia mahitaji ya kibali cha ajira kilichotolewa, ukamilifu wa viambata vilivyohitajika kwa mwombaji, na mwaka wa kuhitimu waombaji; na
ii. Pili, uchambuzi wa kina ulifanyika ukihusisha pia uhakiki wa nyaraka za maombi yaliyopata uzito wa juu, kulingana na vigezo vilivyowekwa.

## 2. KUHUSU UZINGATIAJI WA MAHITAJI NA MSAWAZO SAWA WA WATUMISHI

**Ndugu Wanahabari**

Upangaji wa watumishi wa Kada za Afya na Ualimu katika Vituo vya kutolea huduma za Afya na shule, umezingatia mahitaji ya watumishi katika mikoa husika. Kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** katika kufanya maboresho makubwa ya Sekta ya Afya, upangaji wa watumishi wapya umezingatia mahitaji ya watumishi katika Halmashauri zenye Hospitali mpya, Vituo vya Afya vipya, na Zahanati mpya zilizokamilika ambazo zimeshindwa kutoa huduma za msingi, kutokana na kukosa watumishi wenye sifa, pamoja na Halmashauri zenye upungufu mkubwa wa watumishi hao. Aidha, kwa upande wa kada za Ualimu, utaratibu wa upangaji ulizingatia mgawanyo wa nafasi kwa kila somo, na kiwango cha Elimu kulingana na hitaji la kibali.

**Mchakato huu wa ajira umetoa fursa kwa waombaji kutoka mikoa yote ya Tanzania**, hivyo basi upangaji wake umezingatia uzalendo na utamaduni wetu, **kuwa kila mtanzania anaweza kufanya kazi mahali popote nchini**.

## 3. WAOMBAJI WALIOKIDHI VIGEZO NA KUPANGIWA VITUO

### (a) Waombaji wa Kada za Afya

**Ndugu Wanahabari**

Kwa upande wa kada za Afya, Waombaji wenye sifa waliokidhi vigezo na kupangiwa vituo vya kazi ni **6,876** wanawake ni **3,217** sawa na asilimia **46.8** na wanaume ni **3,659** sawa na asilimia **53.2** wakiwemo wenye ulemavu **42** sawa na asilimia **0.61** kutokana na uchache wa waombaji wenye sifa wa kundi hilo.

Aidha, nafasi **736** kada za Afya zilikosa waombaji wenye sifa. Kada hizo ni Daktari wa Meno **(50),** Tabibu Meno **(43),** Tabibu Msaidizi **(244),** Mteknolojia Mionzi **(86)** na Muuguzi- ngazi ya cheti **(313).** Kada hizi zitarudiwa kutangazwa ili kupata waombaji wenye sifa watakaojaza nafasi hizo.

**Ndugu Wanahabari**

Mchanganuo wa idadi ya wataalamu wa Kada za Afya waliopata nafasi za ajira umeoneshwa kwenye Jedwali la 1.

**Jedwali la 1: Mchanganuo wa Waombaji waliopata ajira wenye Ulemavu na Wasiokuwa na Ulemavu**

| Na. | Kada | Wasiokuwa na ulemavu | Wenye Ulemavu | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Afisa Afya Mazingira Msaidizi Daraja la II | 98 | 2 | 100 |
| 2 | Afisa Lishe Daraja la II | 41 | 1 | 42 |
| 3 | Afisa Muuguzi Daraja la II (NO) | 68 | 2 | 70 |
| 4 | Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II | 178 | 2 | 180 |
| 5 | Afisa Ustawi wa Jamii Daraja la II | 38 | 12 | 50 |
| 6 | Daktari Daraja la II (MD) | 651 | 1 | 652 |
| 7 | Fundi Sanifu Vifaa Tiba (Biomedical Engineering Technician) Daraja la II | 102 | | 102 |
| 8 | Katibu wa Afya Daraja la II | 69 | 1 | 70 |
| 9 | Mfamasia Daraja la II | 102 | | 102 |
| 10 | Msaidizi wa Afya (Medical Attendant) | 392 | 8 | 400 |
| 11 | Mteknolojia - Dawa Daraja la II | 250 | | 250 |
| 12 | Mteknolojia - Maabara Daraja la II | 197 | 3 | 200 |
| 13 | Mteknolojia Msaidizi – Maabara | 149 | 1 | 150 |
| 14 | Muuguzi Daraja la II | 3,074 | 2 | 3,076 |
| 15 | Tabibu Daraja la II (CO) | 1,267 | 6 | 1,273 |
| 16 | Mteknolojia - Mionzi Daraja la II | 34 | | 34 |
| 17 | Tabibu Meno Daraja la II | 69 | | 69 |
| 18 | Tabibu Msaidizi | 55 | 1 | 56 |
| **Jumla Kuu** | | **6,834** | **42** | **6,876** |

**(b)Waombaji wa Kada za Ualimu**

**Ndugu Wanahabari**

Kwa upande wa kada za Ualimu, Waombaji wenye sifa waliokidhi vigezo na kupangiwa vituo vya kazi ni **9,800** ambapo jumla ya walimu **5,000** wamepangwa shule za Msingi na walimu **4,800** Shule za sekondari**,** wakiwemo walimu wenye ulemavu wa shule za Msingi na Sekondari **261.**

Kati ya Walimu **5,000** wa shule za Msingi wanawake ni **2,353** sawa na asilimia **47.06** na wanaume ni **2,647** sawa na asilimia **52.94**. Kwa upande wa walimu **4,800** wa Shule za sekondari wanawake ni **1,289** sawa na asilimia **26.85** na wanaume ni **3,511** sawa na asilimia **73.15.** Aidha, walimu wenye ulemavu **261** wa shule za Msingi na Sekondari walioajiliwa ni sawa na asilimia **2.66** ya walimu wote walioajiliwa wakiwemo wanawake **84** na wanaume **177**. Napenda ieleweke pia kuwa, kwa walimu wa sekondari tumetoa ajira za walimu wa sayansi kwa asilimia **76** ya nafasi **4,800** tulizopewa.

**Ndugu Wanahabari**

Mchanganuo wa idadi ya walimu waliopata ajira kwenye kada mbalimbali za ualimu umeoneshwa kwenye Jedwali la 2.

**Jedwali 2: Idadi ya walimu waliopangwa kuzingatia nafasi zilizoainishwa katika kibali**

| Idara | Kiwango Cha Elimu | Jumla |
|---|---|---|
| Msingi | Bachelor Degree Education (Arts) | 74 |
| | Bachelor of Education in Early Childhood Education | 500 |
| | Certficate in Early Child Education | 15 |
| | Certificate in Primary Education | 2,195 |
| | Certificate in Primary Education - Physical Education | 2 |
| | Certificate in Primary Education - Special Education | 135 |
| | Diploma in Early Child Education | 1,000 |
| | Diploma in Primary Education | 1,000 |
| | Diploma in Secondary Education (Arts) | 79 |
| **Jumla ndogo Msingi** | | **5,000** |
| Sekondari | Bachelor Degree Education (Science) | 1,768 |
| | Bachelor Degree Education (Arts) | 680 |
| | Bachelor Degree Education (Business) | 70 |
| | Diploma in Secondary Education (Arts) | 360 |
| | Diploma in Secondary Education (Business) | 16 |
| | Diploma in Secondary Education (Science) | 1,901 |
| | Diploma in Secondary Education- Physical Education | 5 |
| **Jumla ndogo Sekondari** | | **4,800** |
| **Jumla Kuu** | | **9,800** |

## 4. SHUKRANI KWA MHE. RAIS

**Ndugu wanahabari**

Tunamshukuru sana **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutekeleza sera ya elimu bila ada, ambapo pamoja na mambo mengine, imepelekea watoto ambao walikuwa hawawezi kusoma kutokana na kushindwa kulipiwa ada, kwenda mashuleni. Kutokana na ongezeko la wanafunzi kupitia sera hii, uhitaji wa walimu na miundombinu ya madarasa umeongezeka. Katika kukabiliana na changamoto hii, kwa kipindi cha miezi 15 aliyokuwepo madarakani, Rais wetu mpendwa ametuwezesha kujenga madarasa **15,000** kupitia fedha za mkopo wa IMF, na kutupatia kibali cha kuajiri watumishi wa elimu **9,800** na wa afya **7612.** Aidha, katika mwaka 2020/21 Serikali iliajiri watumishi **23,000** kada ya elimu na afya. **Hatua hizi zinazochukuliwa na Mhe. Rais zinastahili kupongezwa sana**.

## 5. MAELEKEZO YA WAZIRI

**Ndugu wanahabari**

Napenda kutumia fursa hii kutoa maelekezo ya Msingi mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa na Waajiriwa na Waajiri.

a. Waajiriwa wapya wote wahakikishe wanaripoti kwa Wakurugenzi wa Halmashauri walizopangiwa

wakiwa na Kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho ya NIDA, Cheti halisi cha kuzaliwa, Vyeti Halisi vyote vya Taaluma na Utaalamu wa Kazi vya mwajiriwa, ili vihakikiwe na Mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira;

b. Waajiri wote wahakikishe wanapokea vyeti na kuviwasilisha baraza la mitihani kwa ajili ya uhakiki. Wizara ipewe taarifa mara moja **kwa wale watakaokutwa na vyeti ambavyo ni vya kugushi ili hatua kali zichukuliwe**;

c. Waajiri wote wahakikishe watumishi wapya waliopangwa kwenye Halmashauri, wanapewa barua za ajira, na kuripoti kwenye vituo walivyopangiwa tu, na si vinginevyo;

d. Mwajiriwa mpya atakayechukua posho ya kujikimu, na baadaye asiripoti katika kituo chake cha kazi alichopangiwa, atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria;

e. Waajiriwa wapya ambao hawataripoti katika vituo walivyopangiwa ndani ya siku 14, kuanzia tarehe ya tangazo hili, watakuwa wamepoteza nafasi zao ambazo zitajazwa na waombaji wengine wenye sifa, waliopo kwenye Kanzidata (Database) ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

f. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo Waajiriwa wapya wamepangwa, wahakikishe wanawapokea Waajiriwa wapya na kuwawezesha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma, na baadaye kutoa taarifa ya kuripoti kwao. Taarifa za kuripoti waajiriwa hao zijazwe kwenye mfumo wa kielektroniki ***(ajira.tamisemi.go.tz)**,* baada ya kila mtumishi kupokelewa na kukamilisha taratibu;

g. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kukamilisha taratibu za ajira haraka, ili waajiriwa wapya waingizwe kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS) mapema iwezekanavyo;

h. Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri, kuhakikisha wanatekeleza maagizo ya OR-TAMISEMI yaliyotolewa kwenu Mwezi Machi, 2022, ya kuhakikisha mnafanya msawazo wa IKAMA ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, ndani ya Mkoa na Halmasgauri kabla au ifikapo tarehe 30 Juni, 2022. Tekelezeni kwa biddi maelekezo hayo ili kuhakikisha shule zinakuwa na uwiano mzuri wa walimu, na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kabla au ifikapo tarehe **15 Julai, 2022**. OR-TAMISEMI haitasita kumchukulia hatua Mwajiri ambaye hatatekeleza maelekezo haya ya kufanya msawazo wa walimu

katika kuleta uwiano wa mwalimu, na wanafunzi wa **1:60** ulioelekezwa;

i. Tunawaelekeza Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kushirikiana na Bodi zao za shule ili kufuata miongiozo ambayo Wizara imetoa kwa ajili ya michango ya wanafunzi wanaoendelea na masomo. **Hatua kali zitachukuliwa kwa Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu yeyote ambaye ataenda kuinyume na miongozo iliyotolewa na Serikali**; na

j. Walimu waliopo kazini na Waajiriwa wapya, kuhakikisha wanafundisha wanafunzi kwa weledi, na bidii ya hali ya juu kwa kuzingatia kalenda ya ufundishaji iliyopo. Wakuu wa Shule, Waratibu Elimu Kata, Maafisa Elimu wa Halmashauri na Mikoa yote nchini kufuatilia ufundishaji wa kila siku darasani, na kujiridhisha kuwa wanafunzi wanapata umahiri unaotarajiwa kwenye ngazi mbalimbali za elimu ya Msingi na Sekondari.

Aidha, Watumishi wote wa kada za Afya nchini, wanaoendelea na utumishi, na walioajiriwa wapya, kuhakikisha wanawahudumia wananchi kwa weledi na upendo wa hali ya juu, kwa kuzingatia Sheria, kanuni na miongozo ya utoaji bora wa huduma za afya nchini.

**Ndugu Wanahabari**

Majina ya waombaji wote waliopangiwa vituo vya kazi yanapatikana katika Tovuti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI *www.tamisemi.go.tz.*

Asanteni kwa kunisikiliza.



Innocent L. Bashungwa (Mb.)

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI**